

# HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

MKOA WA KILIMANJARO

Simu : 027-2758441  
Fax : 027- 2756102



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

S. L.P. 27  
HAI

Tarehe 20/10/2020.

## TANGAZO LA ZABUNI.

Halmashauri ya Wilaya ya Hai inatangaza zabuni ya kukodisha magari kwa ajili ya kazi maalumu itakayofanyika tarehe 27/10/2020 hadi tarehe 28/10/2020 ndani ya mipaka ya Halmashauri. Magari yanayohitajika ni **FUSO LONG BASE tani 5 na CANTER tani 3** na yanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

1. Liwe na uwezo wa tani 5 (Fuso Long base) na tani 3 (Canter).
2. Liwe na dereva mwenye leseni yenye hadhi ya kuendesha magari ya mizigo.
3. Liwe na Bima hai (Valid Insurance Cover).

### ZABUNI HII INATANGAZWA CHINI YA MASHARTI YAFUATAYO:-

1. Kwa mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuhakikisha gari linafika yadi ya Halmashauri saa 1.30 asubuhi ya tarehe **27/10/2020**.
2. Mwombaji atakayeshinda zabuni awe tayari kupeleka gari lake sehemu yoyote atakayopangiwa ndani ya Wilaya ya Hai.
3. Mwombaji ainishe kwenye maombi yake akionyesha aina ya gari, namba ya usajili, bei ya kukodi gari kwa siku moja, na namba ya simu yake kwa ajili ya mawasiliano.
4. Maombi ya zabuni yafungwe kwenye bahasha na kuandikwa juu pembeni zabuni ya kukodi gari na yatumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni(W), S.L.P 27 Hai na zipelekwe ofisi ya ugavi na manunuzi.
5. Mwombaji wa Zabuni atalazimika kumlipa Dereva wake posho ya kujikimu
6. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya ijumaa tarehe **23/10/2020 saa 8.00 mchana**.
7. Halmashauri ya Wilaya ya Hai hailazimiki kukubali kima cha zabuni cha juu au cha chini.
8. Kazi inayokusudiwa kufanywa na magari haya ni **NYETI** hivyo ni lazima mwombaji ajiridhishe kuwa gari lake liko katika hali nzuri ya kumudu kazi hiyo bila kuharibika.
9. Gari liwe na ubora na safi.

### AINA YA GARI ZINAZOHITAJIKA.

| N/A                               | AINA YA GARI   | UWEZO                       | IDADI |
|-----------------------------------|----------------|-----------------------------|-------|
| 1                                 | Fuso long base | Kuanzia tani 5 na kuendelea | 7     |
| 2                                 | Canter         | Tani 3                      | 10    |
| JUMLA YA MAGARI ( FUSO NA CANTER) |                |                             | 17    |

  
YAHANA E. SINTOO.

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI.  
JIMBO LA HAI.

